


# JIMBO KATOLIKI MOSHI

SHULE YA SEKONDARI URU,  
S.L. P 1512,  
MOSHI.



Barua pepe: [info@urusecondary.sc.tz](mailto:info@urusecondary.sc.tz)  
SIMU NA: 0755 483690

Kumb. Na. USS/UTAW/VOL.I/60/2020

20/06/2020

MZAZI/MLEZI

**YAH: MAELEKEZO MUHIMU KWA WAZAZI KUHUSU KUFUNGUA SHULE**

Nakujulisha kuwa shule inafunguliwa kuendelea na masomo baada ya kufunga tangu tarehe 17/03/2020 kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Corona (COVID -19)

Kulingana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais tarehe 16/06/2020 na pia maelekezo ya nyongeza ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia ya tarehe 17/06/2020 kwamba shule zote zifunguliwe kwa maelekezo ya viongozi wetu mihula imebadilika na kuwa utaendelea hadi tarehe 28/8/2020 na baada ya hapo mihula wa pili utaanza na kuendelea hadi tarehe 18/12/2020. Hata hivyo kwa kipindi chote cha kuanza masomo tarehe 29/06/2020 hadi 18/12/2020 kutaongezwa saa mbili za masomo kwa siku lengo ni kufidia muda uliopotea na kuhakikisha mada zote za mwaka huu zinakamilika.

1. Kwa barua hii nakujulisha kuwa wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti shuleni siku ya Jumamosi tarehe 27/6/2020 kwa maandalizi ili kuanza masomo tarehe 29/06/2020
  - i. Kila mwanafunzi aripoti siku tajwa kuanzia asubuhi hadi saa 11.00 jioni.
  - ii. Kila mwanafunzi aje na barakoa tano zenye rangi ya mfanano wa sweta la kidato chake na ziwekwe alama ya jina lake.
  - iii. Mzazi/mlezi ampatie mwanae mahitaji yote muhimu ya binafsi kwa kadri ya utaratibu.
  - iv. Kila mtoto apime afya ili kujiridhisha juu ya hali ya afya yake.
2. Shule inawahakikishia wazazi na wanafunzi wote usalama wa kiafya na tayari miundombinu sahihi imeshawekwa kwa kadri ya maelekezo ya kujikinga na maambukizi ya corona yaliyotolewa na wizara ya afya.

3. Kikao cha mmiliki wa shule na uongozi wa shule ulikubaliana kuwa wazazi ambao hawakumaliza ada ya muhula wa kwanza utakaoishia tarehe 28/08/2020 wamalizie ada hizo sasa. Fedha zote zilipwe benki.
4. Kutokana na kuathirika kwa pande zote dhidi ya janga la Corona ada ya muhula wa pili imepunguzwa na kuwa kiasi cha Tsh 800,000/= tu. Fedha zote zilipwe benki kwenye akaunti zifuatazo
  - i) MKOMBOZI BANK 00510503545101 Jina la akaunti Uru sekondari
  - ii) NBC BANK 017101000566 Jina la akaunti Uru Sekondari

Kisha stakabadhi ya malipo (pay in slip) itumwe shuleni kwa wakati. Unaweza kulipa kuanzia sasa.

5. Kikao cha wazazi kilichokuwa kimepangwa kufanyika tarehe 01/8/2020 kimeahirishwa na hivyo kitafanyika tarehe 05/9/2020 siku ya Jumamosi saa 4:00 kamili asubuhi. Tumesogeza mbele ili kuwapa nafasi ya kujiandaa vizuri kwani tunatambua hali halisi ya kiuchumi. Niombe kila mmoja ashiriki kwani msingi wa mafanikio ni vikao.

Mwisho, nawatakia maandalizi mema katika kuwaandaa watoto kurudi salama na kwa wakati. Niombe pia ushirikiano wa hali na mali kwa kufuatilia maendeleo ya taaluma na afya za watoto kipindi chote kilichosalia cha mwaka huu.

Tunashukuru sana kwa ushirikiano na tunawatakia kila jema.

Asanteni

Wako katika Kazi



PETER R. OSOKI

MKUU WA SHULE

HEADMASTER  
URU SECONDARY SCHOOL  
P.O. BOX 1512-MOSHI